## Utangulizi

Katika maisha yetu tunaweza kukabiliwa na changamoto nyingi na migogoro kati ya wamiliki wa nyumba/mali na wapangaji. Shida nyingi inatokaana na ukiukwaji wa makubaliano kati ya wamiliki na wapangaji na kusababisha usumbufu kwa mwingine ikiwemo hata kwa majirani.

Lengo kuu la kijarida hiki ni kukuelimisha msomaji juu ya uwajibikaji kati ya Mmiliki na Mpangaji mara tu baada ya kuiingia katika makubaliano ya upangishaji. Tunamatumaini kuwa kijarida hiki kitaweza kukusaidia ili kuweza kupunguza migogoro kati ya Mmiliki na Mpangaji.

Mara tu baada ya kupitia na kusoma kijarida hiki, msomaji anatakiwa aelewe kuwa uhusiano mzuri kati ya Mmiliki na Mpangaji hujengwa juu ya uaminifu kati yao. Kwa mtazamo wa mwenye mali, anapaswa kumuamini Mpangaji

kuwa anaweza kutunza mali na atawajibika kulingana na makubaliano.

## Mmiliki ni nani

Ni Mtu, Kampuni au Taasisi anaye miliki mali ikiwa ni ardhi, jengo au nyumba na ana uwezo wa kupangisha Mtu, Kampuni au Taasisi

## Mpangaji

Ni Mtu, Kampuni au Taasisi anaweza kuchukua mali kama vile ardhi au pango kwa idhini ya Mmiliki wa mali na kupangisha kwa matumizi maalumu kulingana na makubaliano.

## Mkataba wa upangaji

Ni makubaliano kati ya Mmiliki na Mpangaji ambapo Mmiliki anaridhia mali yake kukodishwa na Mpangaji kulingana na matumizi na kodi.

## Wajibu wa mmiliki

1. Kufanya ukarabati wa pango.
2. Kuweka mazingira salama na rafiki kwa binadamu.
3. Kulipa kodi serikalini zitokanazo na pango au ardhi.
4. Kutoa notisi kwa mpangaji.
5. Kuto kuingilia faragha ya mpangaji.

## Wajibu wa mpangaji

1. Kulipa kodi.
2. Kutunza mazingira ya pango au ardhi.
3. Kuruhusu mmiliki kukagua eneo.
4. Kukabidhi pango au ardhi katika hali ambayo alipangishwa.
5. Kuto kuweka rehani, kupangisha na kubadilisha umiliki wa pango.
6. Kutumia pango kwa matumizi yaliyo idhinishwa kwenye mkataba.

| **ANGALIZO** |
| --- |
| Mpangaji atakodisha pango au ardhi aliyopanga endapo kukiwa na ridhaa kutoka kwa Mmiliki |

## Sheria

Sheria ya Ardhi Sheria Na. 4, Sheria ya Mabaraza ya Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi Sheria Namba 2, Sheria ya Udhibiti wa Kodi ya Pango Sheria Na. 7 ya 1984 na Sheria ya Mikataba ni sheria zinazotoa mwongozo zaidi kwenye utatatuzi wa migogoro ya ardhi iliyotokana na migogoro kati ya Mmiliki na Mpangaji.

## Utatuzi wa migogoro

Endapo kutatokea migogoro kati ya Mmiliki na Mpangaji, utatuzi utafauta namna ilivyo ainishwa kwenye mkataba (kama imeainishwa) na pia yanaweza tatuliwa katiak Mabaraza ya Ardhi na Mahakama nchini.

## Hitimisho

Pamoja na mambo mengine mengi, ni muhimu kukumbuka kwamba Mpangaji anaweza kupangisha kama amepata idhini ya Mmiliki. Endapo Mmiliki akitoa notisi ya kuhama, basi ita muathiri Mpangishwaji aliyepangishwa na Mpangaji.

Uhusiano wa Mpangishwaji na Mpangaji utakuwa kama uhusiano wa Mmiliki na Mpangaji kulingana na mkataba waliokubaliana.

Katika kitini hiki, ni matumaini ya Kituo kuwa umepata mwanga wa kutosha kuelewa mahusiano ya kisheria kati ya Mmiliki na Mpangaji. Kwa ushauri zaidi unaweza kufika katika ofisi zetu za msaada wa sheria.

